

**Tunapaswa Tuitweje Kama  
Wafuasi Wa Kristo?  
(What Are We To Be Called As  
Followers Of Christ?)**

**Na**

**John Kombo**

# **Tunapaswa Tuitweje Kama Wafuasi Wa Kristo?**

**Na**

**John Kombo**

**Aprili 11, 2015**

# Tunapaswa Tuitweje Kama Wafuasi Wa Kristo?

Watu wengi wanadai kuwa ni Wakristo alafu bado wanajiita kwa majina tofauti na kufundisha mafundisho tofauti. Kama sisi ni Wakristo wa kweli, kama jinsi Agano Jipya linavyotafsiri neno hilo, tunapaswa kuzidisha mambo mengine katika jina hilo tulilopewa na Mungu? (mifano mingine inaweza kuwa: mkristo wa Katholiki, mkristo wa Kibaptisti, mkristo wa kimethodisti, nk).

Watu wa Mungu chini ya Agano la Kale waliitwa Waisraeli (Mwa. 35:10). Mungu akasema siku moja watu wake wataitwa kwa majina mapya. (Isa. 62:2). Haki ya Mungu ilionyeshwa kwa kumtuma Mwana wake, ambaye katika yeye tunaweza kuwa na imani. (Rum. 3:22).

Injili ya Yesu Kristo ilikwenda kwa Waisraeli mwanzo tu wa Agano Jipya. (Mat. 10:6).

Hili lilikuwa Taifa teule la Mungu. Katika Mdo 11:18, Petro na wale aliokuwa nao walielewa kwamba Mungu kwanzia wakati huo na kuendelea alitoa toba sio tu kwa Wayahudi pekee lakini pia kwa Mataifa pia. Hii ili timiza unabii katika Isa. 62:1-2; 65:15.

Mtu yeyote alipoelewa (Myahudi au Mtaifa) angeokoka, ulikuwa ni wakati wa jina jipya la Mungu kwa watu wake kuanza kutumika. Jina jipya lina kuja Antiokia, baada ya unabii huu kutimizwa. Rekodi inapatikana katika Mdo. 11:26. Mitume waliitwa kwanza Wakristo hapo Antiokia. Mungu anataka sisi sote tuitwe Wakristo, kwa sababu inamtukuza. (2 Thes. 1:12).

Je hatupaswi kuvaa jina la mwanadamu awaye yote? Jibu ni hapana. Mtume Paulo aliwaandikia kanisa la Korintho, *“Basi maana yangu ni hii, ya kwamba kila mtu wa kwenu kusema, mimi ni wa Paulo, na mimi ni wa Apolo, na mimi ni wa Kefa, na mimi ni wa Kristo. Je! Kristo amegawanyika? Je! Paulo alisulubiwa kwa ajili yenu? Au je! Mlibatizwa kwa jina la Paulo?”*

Kristo amegawanyika? Au Paulo alisulubiwa kwa ajili yenu? Au mlibatizwa kwa jina la Paulo? (1 Kor. 1:12-13).

Majina tofauti ambayo watu hutumia zinaleta mgawanyiko miongoni mwa wale wanaodai wanamfuata Bwana wetu Yesu. Kuna zaidi ya madhehebu 200 tofauti duniani. Hii ni kinyume na maombi ya Bwana wetu katika Yohana 17:20-23.

Sote tunaweza kuwa Wakristo na Wakristo pekee.

Mungu awabariki wale wanaojitahidi kuitwa tu Wakristo.

John Kombo Nandwa  
Kanisa la Kristo Baruti  
Nakuru, Kenya











